

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

636

TEHAMA

Muda: Saa 3

Jumatano, 9 Mei 2012 mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu B.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Kwa kutumia mifano dhahiri, eleza kwa ufupi aina za njia za mawasiliano.
2. Bainisha faida za matumizi ya vipindi vya radio katika kufundishia masomo mbalimbali.
3. Fafanua hatua tano zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kufundisha mada ya usikivu kwa wanafunzi wako.
4. Eleza dhana ya neno katalogi kisha bainisha umuhimu wake.
5. Fafanua vipengele muhimu vya muhtasari wa somo.
6. (a) Bungua bongo ni nini?
(b) Bainisha faida mbili za matumizi ya bungua bongo katika kufundisha mada ya matumizi ya maktaba.
7. Eleza kwa kifupi sifa nne za zana za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA.
8. (a) Nini maana ya zana za kufundishia?
(b) Taja makundi matatu ya zana za kufundishia na toa mfano mmoja kwa kila kundi.
9. Taja vifaa vinne vinavyoweza kutumika katika mawasiliano wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
10. (a) Mawasiliano kwa njia ya alama ni nini?
(b) Ainisha makundi makuu matatu ya alama za barabarani.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu hii.

11. Kwa kutumia mifano, eleza kazi za schemu kuu zinazounda mfumo wa Kompyuta.
12. Tathmini mambo muhimu matano yanayotakiwa kuwepo ili wanafunzi waweze kujifunza kwa ufanisi.
13. Fafanua vigezo vitano vinavyoweza kutumika kuangalia uwezo wa mwali muwanafunzi wakati wa kufundisha somo la mfano.

14. Kwa kutumia mifano mitano elezea umuhimu wa kufanya upimaji kwa mwalimu wa somo la TEHAMA.
15. Eleza mambo yasiyopungua matano yanayotakiwa kuzingatiwa wakati wa kuandaa andalio la somo la TEHAMA.
16. Tathmini ukitoa hoja zisizopungua tano umuhimu wa kufundisha kwa kutumia TEHAMA.
17. Fafanua mambo matano anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA wakati anapofundisha kwa kutumia zana za kufundishia darasani.
18. Eleza namna mwalimu anavyoweza kufundisha stadi ya kutuma ujumbe wa faksi kwa kutumia onesho mbinu kama njia ya kufundishia.